**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

*Dar es Salaam*
*02 Februari, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

## TAARIFA KWA UMMA

## RAIS SAMIA KUSHIRIKI MKUTANO WA DUNIA WA SERIKALI 2026 NA UZINDUZI WA GLOBAL AFRICA INVESTMENT SUMMIT

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, atashiriki katika uzinduzi wa *Global Africa Investment Summit (GAIS)* utakaofanyika sambamba na Mkutano wa Dunia wa Serikali *(World Governments Summit – WGS)* 2026 wenye kaulimbiu ***"Kutengeneza Serikali Zijazo (Shaping Future Governments)"*** utakaofanyika Dubai, Falme za Kiarabu (UAE).

Mkutano wa WGS ndio lengo kuu la ziara hii, wakati GAIS ni mpango wa ngazi ya juu unaoendeshwa pembeni mwa WGS, ukiwa ni juhudi iliyoanzishwa na Dkt. Akinwumi Adesina, Rais Mstaafu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, kwa kushirikiana na wadau wa kimataifa, kwa lengo la kuunganisha miradi yenye tija barani Afrika na wawekezaji wa kimataifa.

Mkutano wa Dunia wa Serikali *(World Governments Summit – WGS)* ni jukwaa la kimataifa linaloandaliwa kila mwaka na Serikali ya Falme za Kiarabu, likiwa linawakutanisha Wakuu wa Nchi na Serikali, watunga sera, viongozi wa taasisi za kimataifa, sekta binafsi, wasomi na wabunifu wa sera kutoka duniani kote.

WGS hulenga kujadili na kuunda mwelekeo wa baadaye wa utawala wa serikali, sera za umma, mageuzi ya kiuchumi, matumizi ya teknolojia, pamoja na namna serikali zinavyoweza kuhimili mabadiliko ya dunia na kuchochea maendeleo endelevu.

WGS 2026 inalenga kuoanisha maamuzi ya kisera na mwelekeo wa mitaji ya kimataifa, kwa kuzingatia masuala ya uthabiti wa kiuchumi, usimamizi bora wa rasilimali, ubunifu wa sera, na mchango wa serikali katika kuharakisha uwekezaji na ukuaji wa uchumi.

Katika kipindi cha mkutano huo, Rais Samia anatarajiwa kufanya mazungumzo ya kiserikali na nchi mwenyeji – Falme za Kiarabu (UAE), pamoja na kukutana na viongozi wa taasisi za fedha za kimataifa na wawekezaji wakubwa, hatua inayolenga kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi na kuvutia mitaji ya uwekezaji nchini.

Ushiriki huu unaendana kikamilifu na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (DIRA 2050) pamoja na Sera Mpya ya Mambo ya Nje, zinazosisitiza diplomasia ya kiuchumi kama mhimili mkuu wa mahusiano ya kimataifa ya Tanzania.

Hii ni ziara ya kwanza ya kimataifa kwa Rais Samia baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2025, ikiiakikishia jumuiya ya kimataifa uthabiti wa kisiasa, mwendelezo wa sera na dhamira ya Tanzania katika kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI).

Uamuzi wa kuanza ziara ya kwanza ya kimataifa kupitia Mkutano wa Dunia wa Serikali (WGS), badala ya ziara ya kawaida ya kiserikali, unatokana na kipaumbele cha Serikali katika siku 100 za mwanzo za muhula wa pili wa Awamu ya Sita, ambapo mkazo mkubwa umewekwa katika kuharakisha uundaji wa ajira kupitia ongezeko la uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje.

WGS ni miongoni mwa majukwaa machache duniani yanayowaweka pamoja kwa wakati mmoja watunga sera, wamiliki wa mitaji na wawekezaji wa kimkakati, hivyo kutoa fursa ya kuoanisha vipaumbele vya kitaifa na maamuzi halisi ya uwekezaji.

Kufanikisha hilo, GAIS inalenga kuoanisha miradi iliyo tayari kwa uwekezaji na wawekezaji wenye uwezo wa kifedha, kwa kuzingatia sekta za kipaumbele kama nishati, miundombinu, kilimo-biashara, viwanda, teknolojia na usafirishaji. Kwa Tanzania, jukwaa hili ni fursa ya kuwasilisha miradi yenye tija moja kwa moja kwa wawekezaji wanaofanya maamuzi ya uwekezaji.

Kuanzia katika jukwaa la WGS kunaiwezesha Tanzania kuwasilisha miradi yake yenye tija na ya kimkakati mapema, kuwa na mazungumzo ya moja kwa moja na wawekezaji wakubwa, na kuweka msingi wa matokeo ya haraka yanayochangia ajira, ukuaji wa uchumi na utekelezaji wa DIRA 2050.

Katika WGS 2026, Rais Samia anatarajiwa kushiriki mjadala wa Wakuu wa Nchi na Serikali wenye mada ***"Serikali na Mustakabali wa Uwekezaji: Mtazamo wa Afrika"***, utakaowakutanisha Mheshimiwa João Lourenço, Rais wa Angola na Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika; Mheshimiwa John Dramani Mahama, Rais wa Ghana; pamoja na Dkt. Akinwumi Adesina, Rais Mstaafu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Mjadala huo utazingatia mwelekeo mpya wa maendeleo ya uchumi wa Afrika, namna ya kuhamasisha uwekezaji wa kimataifa, na kuharakisha mabadiliko ya bara kutoka utegemezi wa misaada kwenda ukuaji unaoongozwa na uwekezaji.

**MAELEZO KWA MHARIRI**

World Governments Summit (WGS) ni jukwaa la kimataifa linalowaunganisha watunga sera na wamiliki wa mitaji, na ndilo eneo kuu la kuendeshea diplomasia ya kiuchumi kwa mtazamo wa kimkakati.

Global Africa Investment Summit (GAIS) ni jukwaa la kimkakati la deal-making linalofanyika sambamba na WGS, likiwa na lengo la kubadilisha majadiliano ya sera kuwa uwekezaji halisi unaotekelezeka. GAIS imeanzishwa na Dkt. Akinwumi Adesina kwa kushirikiana na wadau wakuu wa kimataifa wa uwekezaji.

Ushiriki wa Rais katika mkutano huu unaakisi utekelezaji wa DIRA 2050 na Sera Mpya ya Mambo ya Nje, kwa kuweka kipaumbele diplomasia ya kiuchumi inayolenga matokeo ya moja kwa moja badala ya ziara za kawaida za kiserikali.

Kwa Tanzania, GAIS inatoa fursa ya kuvutia wawekezaji kwa miradi iliyo tayari, kuongeza uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI), na kuimarisha nafasi ya nchi kama kituo cha uwekezaji wa muda mrefu barani Afrika.

Aidha, Rais anatarajiwa kufanya mazungumzo ya kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi na viongozi wa nchi mwenyeji, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) pamoja na Viongozi wa taasisi za fedha na wawekezaji wakubwa duniani.

Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu